# WILAYA YA NANDI

## DARASA LA NNE MUHULA WA TATU

PENPLUS NANDI

## KISWAHILI

**Muda: Saa 1 Dakika 40**

**Jaza mianya kwa majibu sahihi kwa swali 1-15.**

Kuku ___1___ mayai ___2___ sana. Mayai hayo yaliwekwa kwenye choto kisha ___3___ kwa muda wa ___4___ matatu hivi kisha ___5___ vifaranga ___6___ walikuwa na rangi tofauti. Kuku alilinda vifaranga ___7___ wasiliwe na ___8___.

Siku ___9___ kuku aliwaficha vifaranga kwenye mbawa ___10___. Mwewe naye alifanya ujanja na kuangusha punje ___11___ mahindi karibu. Kuku ___12___ na kuangukia kwenye mlo wake. Kuku huyo ___13___ mahindi kwa furaha bila kufahamu ujanja wa mwewe. Mwewe aliwavamia vifaranga na kumchukua ___14___. Kuku alimlilia kifaranga wake lakini kilio si ___15___.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. alizaa | B. aliangua | C. alitaga | D. aliteka |
| 2. | A. mengi | B. mingi | C. wengi | D. mwingi |
| 3. | A. aliyalalia | B. akayaatumia | C. akayavamia | D. akayakalia |
| 4. | A. wiki | B. juma | C. miezi | D. majuma |
| 5. | A. yakaanguliwa | B. yakaliwa | C. yakatolewa | D. yakatozwa |
| 6. | A. ambavyo | B. ambayo | C. ambaye | D. ambao |
| 7. | A. wake | B. vyake | C. vyao | D. zao |
| 8. | A. jogoo | B. mbuni | C. mwewe | D. njiwa |
| 9. | A. mmoja | B. kimoja | C. moja | D. mocha |
| 10. | A. yake | B. zake | C. yao | D. lao |
| 11. | A. la | B. ya | C. za | D. wao |
| 12. | A. alipuruka | B. alianguka | C. alidandia | D. alizama |
| 13. | A. alitafuna | B. alikekela | C. aliyadona | D. aliyagegeda |
| 14. | A. kimoja | B. mmoja | C. moja | D. wamoja |
| 15. | A. kizuri | B. dawa | C. tatizo | D. kibaya |

**Jibu maswali nambari 16 - 30 kwa kufuata maagizo yaliyotolewa.**

16. Andika sentensi hii katika wingi;
    Ubao utavunjika.
    A. Bao zitavunjika
    B. Mabao yatavunjika
    C. Bao yatavunjika
    D. Mbao zitavunjika

17. Kanusha; Sisi hula asubuhi.
    A. Sisi hatukuli asubuhi.
    B. Sisi hatulangi asubuhi
    C. Sisi hatuli asubuhi.
    D. Sisi hukula asubuhi

18. Alinunua kalamu ________ wino mwekundu.
    A. chenye B. mwenye
    C. lenye D. yenye

19. Chagua kiulizi sahihi;

Amefunga mlango kwa ufunguo

__________?

A. upi B. lipi

C. ipi D. zipi

20. Daktari huitwa tabibu au _______

A. muuguzi B. nesi

C. mganga D. mchawi

21. Chagua kiambishi sahihi.

Chungu __________ ko mekoni.

A. i B. li C. u D. ki

22. Jaza pengo;

Wayo ni kwa mwanadamu, ________ ni kwa ng'ombe.

A. kiatu B. mguu

C. teke D. kwato

23. Kamilisha methali ifuatayo.

Baada ya kisa ni ____________

A. faraja B. kifo

C. mkasa D. kitendo

24. Jina 'dawati' liko katika ngeli gani?

A. LI-YA B. I-ZI

C. U-ZI D. YA - YA

25. Tumia idadi ifaayo;

Wakulima __________ watasafiri.

A. wasita B. kumi na moja

C. wakumi D. wanane

26. Kinda ni mtoto wa ___________

A. ndege B. kuku

C. nyoka D. mbwa

27. Taja jina la umbo hili;



A. Moyo B. Roho

C. Mapenzi D. Kopa

28. Mtu asiyeweza kusikia huitwaje?

A. Kipofu B. Kiwete

C. Kibyongo D. Kiziwi

29. Tunaliitaje jiko la makaa?

A. Meko B. Stima

C. Seredani D. Dohani

30. Tegua kitendawili kifuatacho.

Nyumba ya baba ina wageni wengi.

A. Soko B. Kanisa

C. Shule D. Ulimwengu

**Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali 31 - 40.**

Hapo zamani wanyama walikuwa wakishiriki katika michezo mbalimbali mara moja kwa mwaka. Wakati huu wa michezo, kila mnyama, ndege na hata samaki walikuwa wanaalikwa na mfalme tembo.

Wanyama hawa walikuwa wanashiriki katika michezo mbalimbali kama vile kushindana mbio, kuogelea, kupigana ngumi na mateke na michezo mingineyo.

Pundamilia alikuwa anashinda kila mara katika mchezo wa kupigana mateke. Mbuni naye alikuwa akishindana mbio zote. Rekodi ya papa katika kuogelea iliwashinda wengi kuivunja.

Kila mwaka, mheshimiwa kinyonga alikuwa akialikwa kuja kushabikia mchezo wake wa kupigana ngumi na mateke. Alikuwa akiupenda kama chanda na pete. Katika mchezo huu, kinyonga alipata maarifa mengi hasa siku ile. Pundamilia alimshinda simba kwa kumpiga teke lililomuumiza.

Michezo ilipofika kikomo saa kumi na moja siku hiyo, washindi wakatangazwa na katibu bwana Ngiri na kutuzwa zawadi kochokocho.

31. Wanyama walikuwa wakifanya michezo mara ngapi kwa mwaka?
A. Mbili
B. Moja
C. Tano
D. Kumi

32. Kulingana na taarifa ni mchezo upi ambao haukupendwa na wanyama?
A. Kuogelea
B. Mbio
C. Kupigana
D. Kuimba

33. Ni nani aliyekuwa mshindi katika mchezo wa kupigana mateke?
A. Pundamilia
B. Simba
C. Kinyonga
D. Papa

34. Kulingana na hadithi, makao yake papa ni wapi?
A. Mitini
B. Nyumbani
C. Majini
D. Mwituni

35. Ni wakati gani katika michezo ambao kinyonga alipata maarifa mengi?
A. Pundamilia alipomshinda simba
B. Simba alipomshinda pundamilia
C. Papa alipoogelea akashinda
D. Mbuni alipomshinda ngiri.

36. Mbuni alipokea zawadi kwa kushinda mchezo upi?
A. Kuogelea
B. Mbio
C. Kuimba
D. Kucheza

37. Neno 'kochokocho' limetumika katika ufahamu. Neno hii lina maana ya __________
A. chache
B. ndogo
C. kwa wingi
D. tele

38. Ni nani aliyekuwa katibu wa mchezo mwaka huo?
A. Papa
B. Kinyonga
C. Ngiri
D. Ndovu

39. Neno lenye maana sawa na 'tembo' ni __________
A. ndovu
B. simba
C. mbuni
D. papa

40. Kichwa mwafaka cha hadithi hii ni __________
A. Hapo zamani
B. Wanyama na mbuni
C. Siku ya michezo ya wanyama
D. Kupigana mateke

**Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali 41 - 50.**

Nyoteyo ni msichana mwenye umri wa miaka kumi na miwili. Ana bidii sana masomoni, hata wanafunzi wanzake humwita 'nyota'.

Nyoteyo hana wazazi, yeye ni yatima. Yeye ni mwanafunzi katika shule ya msingi ya Naelewa. Wazazi wake waliaga dunia walipovamiwa na wezi nyumbani kwao miaka mitatu iliyopita. Yeye huishi na mjomba wake.

Nyoteyo hupenda rafiki safi. Hapendi kukaa na watoto wachoyo, wachafu, wanaonuka kama beberu, wezi na wasiofanya kazi za walimu. Hupenda kusoma vitabu vingi vya kiswahili na hadithi nzuri. Yeye husema kuwa akimaliza masomo yake angependa kuwa mhubiri ili awahubirie watu amani. Jambo hili ni tofauti na mahitaji ya wenzake.

Kwa kweli hapendi vita. Yeye ni mpole kama mwanakondoo. Huwauliza walimu wake maswali katika masomo yake. Sasa Nyoteyo ndiye kiranja wa darasa lake la tano. Alichaguliwa na mwalimu wake Bwana Furaha kwa sababu ya tabia zake za kuwapendeza wengi. Ni wangapi wangetamani kuwa na tabia kama za Nyoteyo?

41. Nyoteyo alikuwa na miaka mingapi wazazi wake walipokufa?
A. Kumi na miwili
B. Sita
C. Tisa
D. Kumi

42. Ni akina nani waliowaua wazazi wa Nyoteyo?
A. Majabazi
B. Wezi
C. Wachawi
D. Askari

43. Nyoteyo hapendi ________
A. wanafunzi wanaofanya kazi ya mwalimu.
B. wanafunzi wanaonukia
C. wanafunzi wasiooga
D. wanafunzi wanaowatii walimu wao

44. Kulingana na hadithi hii ni kweli kuwa ________
A. Nyoteyo ni msomaji bora wa vitabu vya kiswahili.
B. Nyoteyo si yatima.
C. Nyoteyo anaishi peke yake kwake
D. Nyoteyo hupenda kukaa na wanafunzi wachoyo

45. Nyoteyo ni mpole kama ________
A. maji  B. mwanakondoo
C. yatima  D. wazazi wake

46. Tunamaanisha nini tunaposema kuwa "Nyoteyo ni yatima"?
A. Hapendi wanafunzi wabaya
B. Yeye ni mwerevu na hana hatia
C. Anasoma kwa bidii
D. Hana wazazi

47. Nyoteyo anatamani kuwa nani atakapomaliza masomo yake?
A. Daktari
B. Mwimbaji
C. Msomaji
D. Mhubiri

48. Nani aliyemchagua Nyoteyo kuwa kiongozi wa darasa lake?
A. Wanafunzi
B. Bwana Furaha
C. Kiranja
D. Wazazi

49. Nyoteyo alikuwa akiishi kwa ________ wake.
A. rafiki  B. mjomba
C. mwalimu  D. wanafunzi

50. Hadithi hii inatufundisha nini?
A. Usiposoma utapita.
B. Tuwe na upendo na amani maishani.
C. Kila mwanafunzi ni yatima.
D. Tusiwaulize walimu maswali mengi darasani